

BAGAMOYO INTERNATIONAL FESTIVAL OF ARTS AND CULTURE

AT BAGAMOYO HISTORICAL TOWN

Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo hufanyika kila mwaka mwezi Oktoba katika mji mkongwe na wa kihistoria wa Bagamoyo - mji wenye historia adhimu na vivutio lukuki nya urithi wa utamaduni wa Mtanzania vinavyotambuliwa na Shirika la UNESCO. Tamasha hili huandaliwa na kuendeshwa na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa); Taasisi inayotoa mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa vijana wenye vipaji. Wakati wote wa Tamasha, maeneo yote ya TaSUBa hupambwa na kazi za sanaa na maonesho mbalimbali ya sanaa. Wasanii mahiri kutoka sehemu mbalimbali za Dunia ambao hufika kuonesha kazi zao za ubunifu wa hali ya juu. Aidha, Tamasha hili huvutia watazamaji, wadau na wapenzi wa sanaa kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lilianza mwaka 1981 kwa kushirikisha kazi za sanaa za wanafunzi na walimu wa TaSUBa pekee. Hata hivyo limeendelea kukua na kuwa maarufu sana na kuchukua sura ya Kitaifa kiasi cha kuwavutia watazamaji na wasanii wengi kutoka mataifa mbalimbali, hivyo kulifanya liwe la Kimataifa zaidi. Zaidi ya vikundi nya sanaa/ wasanii 1,500 wamepata nafasi ya kushiriki kwenye Tamasha hili tangu lianz; katika ya hawa, vikundi nya sanaa/ wasanii 1,300 wakiwa ni wa ndani na 200 ni kutoka nchi mbalimbali. Tamasha hili pia limekuwa kivutio kikubwa kwa watazamaji vijana kutoka katika shule na vyuo mbalimbali nya hapa nchini.

Lengo kuu la Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo ni kutoa nafasi kwa wasanii wa ndani ya nchi na wale kutoka nje kukutana na kusherehekeea uanuai wa utamaduni unaochagiza mshikamano na bunifu mbalimbali. Malengo mahsus ya Tamasha ni haya yafuatayo:

- ✓ Kutoa nafasi kwa wanachuo wa TaSUBa na vyuo vingine kuonyesha kazi zao za sanaa ili kudhihirisha stadi au ujuzi waliopata kutoptaka na mafunzo ya taaluma ya sanaa na utamaduni.
- ✓ Kutoa fursa kwa wasanii wa ndani na nje ya nchi kukutaana na kujenga mahusiano ya uendeshaji wa kazi za kisanii na utamaduni na kusherehekeea uanuai katika Nyanja mbalimbali za sanaa na utamaduni.
- ✓ Kutoa nafasi kwa wasanii vijana kuonyesha vipaji vyao kupitia njia ya sanaa.
- ✓ Kuonyesha na kutangaza sanaa na utamaduni wa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika mashariki.
- ✓ Kutoa nafasi kwa wasanii hasa vijana kuweza kukutana, kubasilishana uzoefu katika kukuza vipaji vyao nya sanaa na utamaduni.

Mbali na kukusanya wasanii maarufu wa ndani na nje, Tamasha hili hutoa nafasi ya kuonyesha sanaa za ufundi na vifaa vingine nya kiutamaduni, vyakula nya asili, kutembelea vivutio nya kitalii nchini Tanzania, michezo ya watoto na mafunzo mafupi mafupi ya utengenezaji au uandaaji wa sanaa.

Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo huandaliwa na:

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

Barabara ya Kaole, S. L. P 32, Bagamoyo, Tanzania

Barua Pepe: info@tasuba.ac.tz / tasuba@michezo.go.tz Wavuti: www.tasuba.ac.tz